# Matukio ya SUA

CHUO KIKUU CHA
SOKOINE CHA KILIMO

Julai - Septemba, 2023




Ardhi ni Hazina

# SUA yapongezwa kwa kuandaa wahitimu bora katika sekta ya kilimo nchini



*Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Mhe. Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba akiongea na Waandishi wa Habari, (hawapo pichani).*

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Mhe. Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba amesifu kazi nzuri inayofanywa na SUA katika kutoa elimu kwa wataalam mbalimbali wa kilimo ambao wamekuwa kichocheo katika kuinua Sekta ya kilimo nchini.

Alibainisha hayo nyumbani kwake jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mchango wa SUA kwenye sekta ya kilimo.

Mhe. Warioba amesema kuwa wakati Tanzania inapata uhuru wataalam katika sekta mbalimbali ikiwemo ya kilimo walikuwa wachache sana hata hivyo jitihada mbalimbali zilianzishwa na serikali ili kupata wataalam katika sekta hizo na hapo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kilianzishwa na baadae Chuo cha Kilimo Morogoro kikiwa chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambapo miaka michache baadae kikawa Chuo Kikuu kamili kinachotoa wataalam wa kilimo.

''Kilimo ni uti wa mgongo wa nchi hii na kwa wakati huo tulikitegemea sana nadhani tulipopata uhuru tulikua na wataalam wachache, kwa mafano nyanja zingine kama uhandisi walikua wawili tu, na madaktari walikua wachache sana, na kwa kilimo kulikua na maafisa ugani kwa ngazi za chini hivyo ilionekana kuna umuhimu wao tukaona tuanzishe mafunzo ya juu kwa upande wa kilimo na hapo ndipo baadhi ya vitengo vilivyoanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mojawapo kilikuwa ni kitengo cha Kilimo", amesema Mhe. Warioba.

Aidha Mhe. Warioba alisema kuwa kutokana na umuhimu mkubwa wa wataalam wa kilimo Serikali iliamua kuendeleza Idara ya Kilimo kuwa Chuo Kikuu kamili ili ishughulikie eneo la kilimo pekee na hivyo michakato ikaendelea na hatimae ilipofika mwaka 1984 bunge likapitisha sheria ya kuanzishwa Chuo Kikuu cha Morogoro ambapo baada ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu Hayati Edward Moringe Sokoine kwa heshima ya Waziri Mkuu huyo kikapewa jina lake la Sokoine.

Jaji Warioba aliendelea kusema kuwa SUA imekuwa ikifanya kazi zake kuu tatu ikiwemo kutoa mafunzo kwa nadharia na vitendo pamoja na kufanya tafiti mbalimbali za kilimo ambapo kitaendelea kufanya hivyo na pia kuendelea kutoa ushauri katika maeneo hayo kwa kuwa yanayokwenda kwa pamoja.

Vilevile alisema SUA imekua Chuo Kikuu pekee nchini kinachojikita katika masuala ya kilimo kwa upana wake na katika kipindi hiki ambacho hali ya hewa duniani inabadilika ndio umuhimu wa SUA unapozidi kuongezeka kwa kuwa wameendelea kuhakikisha wakulima nchini wanalima kwenye majira ya aina yoyote ile iwe kiangazi au masika hasa katika kipindi hiki ambapo dunia inakabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mhe. Jaji Warioba aliipongeza SUA kuanzisha mashamba darasa yaliyopo ndani ya Chuo na kusema kuwa mafunzo kwa vitendo yanaonesha mfano wa namna shamba linavyotakiwa kuwa, na pia uwepo wa mabwawa ya Samaki, na karakana ambayo yamekuwa msaada kwa wanafunzi wanaosoma SUA, vilevile amefurahishwa na uwepo wa mpango wa Atamizi kwa vijana na hivyo SUA kuwa mfano wa vitendo na wahitimu wengi watakuwa vizuri kwenye eneo la vitendo.



**Ardhi ni Hazina**

# Watumishi Kampasi ya Solomon Mahlangu wahimizwa Kushirikiana kutekeleza majukumu yao



**Prof. Raphael T. Chibunda**
Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Watumishi wa SUA wamehimizwa kushirikiana katika utekelezaji wa majukumu na utendaji kazi ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wanafunzi na wanajumuiya wa Chuo

Wito huo ulitolewa na Makamu Mkuu wa Chuo hicho Prof. Raphael Chibunda wakati akiongea na watumishi wa Chuo, Kampasi ya Solomon Mahlangu akiwa katika ziara ya kutembelea Kampasi na Ndaki mbalimbali kwa ajili ya kusikiliza changamoto na kuelezea mipango ya Chuo kwa mwaka ujao wa masomo 2023/2024.

Prof. Chibunda akiwa ameambatana na Menejimenti ya Chuo hicho, alihimiza kila mtumishi kuona umuhimu wa kushirikiana kiutendaji bila ya kushushiana heshima wakati inajengwa nyumba moja.

"Tuendelee kufanya kazi kwa umoja, hakuna haja ya kushindana kwani kila mmoja ana mchango katika utoaji wa huduma kwenye eneo lake", alisema Prof. Chibunda.

Aidha, Makamu huyo wa Chuo alisisitiza kuwa Chuo kitaendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili watumishi wa Chuo hicho pamoja na kuboresha mazingira ya utoaji wa taaluma ili kuendelea kuifanya SUA kuwa bora katika kuandaa wahitimu wenye uwezo mkubwa katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali.

Kwa upande wake, Kaimu Rasi wa Ndaki ya Sayansi Asilia na Tumizi Dkt. Beda Mwang'onde amemshukuru Makamu Mkuu wa Chuo kwa kutenga muda kuzungumza na watumishi akisema kikao hicho kitakuwa chachu katikakuongeza ari ya utendaji kazi kwa watumishi.

Dkt. Neema Sumari ni Mhadhiri na miongoni mwa wafanyakazi walioshiriki katika kikao hicho akiongea na SUAMEDIA amebainisha kuwa kikao hicho kimekuwa na tija kwani changamoto mbalimbali zinazowakabili watumishi zimepatiwa ufumbuzi na nyingine zimechukuliwa kwa ajili ya kutafuta suluhu zaidi.

***"Tuendelee kufanya kazi kwa umoja, hakuna haja ya kushindana kwani kila mmoja ana mchango katika utoaji wa huduma kwenye eneo lake",***



# Wananchi Madaba waipa SUA ardhi kujenga Kiwanda

***"Hivi Sasa Serikali inahimiza vyuo kuongeza mapato yake ya ndani ili viweze kujiendesha badala ya kutegemea ruzuku ya serikali na sisi kama Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo tumebobea kwenye masuala ya misitu na kupitia uzoefu wetu tulioupata kwenye Msitu wetu wa Olmotonyi kule Arusha tumeona tuje kuwekeza hapa Madaba na tunaamini tutakuwa mfano kwa vyuo vingine"***



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala akitoa salamu za SUA kabla ya kusaini Mkataba.*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimesaini Mkataba rasmi na Halmashauri ya Wilaya ya Mdaba Mkoani Ruvuma wa umiliki wa Shamba la Hekta 10,000 kwa ajili ya kilimo cha miti na mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wake na jamii.

Akizungumza kabla ya kusaini Mkataba huo kwenye ukumbi wa Halmashauri hiyo Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Taaluma Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala kwa niaba ya Makamu Mkuu wa Chuo, alisema lengo la shamba hilo ni kwa ajili ya mafunzo pamoja na kuongeza mapato.

"Hivi Sasa Serikali inahimiza vyuo kuongeza mapato yake ya ndani ili viweze kujiendesha badala ya kutegemea ruzuku ya serikali na sisi kama Chuo Kikuu cha Sokoine tumebobea kwenye masuala ya misitu na kupitia uzoefu wetu tulioupata kwenye Msitu wetu wa Olmotonyi kule Arusha tumeona tuje kuwekeza hapa Madaba na tunaamini tutakuwa mfano kwa vyuo vingine" alieleza Prof. Mwatawala.

Alisema kuwa kasi ya upandaji wa miti kwenye shamba hilo la Ifinga imeongezwa nguvu sasa na Mradi wa HEET ambao umetenga fedha kwajili ya kupanua shamba hilo na kuongeza idadi ya miti itakayopandwa ambapo kwa mwaka huu pekee wanatarajia kupanda hekta 500.

Prof. Mwatawala alisema eneo la shamba walilolichukua baada ya kulipa fidia wananchi kwenye kijiji cha Magingo kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kuchakata mazao hayo ya mistu na kuongeza thamani kutaleta maana endapo kiwanda hicho kitapata miti ya kuchakata hasa kutoka kwenye shama hilo.

Akitoa salamu za Wilaya ya Madaba Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya hiyo Bw. Sajidu Idrisa alisema anaamini ujio wa SUA sio tu kwamba utasaidia kuchochea kasi ya upandaji wa miti lakini pia utasaidia kuongeza kipato kwa wananchi watakaoajiriwa kwenye shamba hilo lakini pia vijiji na Halmashauri.



*Msitu wa Mafunzo wa Ifinga uliopo Madaba mkoani Ruvuma*

# Benki ya Dunia waridhika na utekelezaji wa miradi wanayoifadhili SUA



***Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia Nchini Tanzania Bw. Nathan Belete (wa tatu kulia) akiapata maelezo kutoka kwa Prof. Appiah Massawe alipotembelea Kituo cha Umahiri cha mashariki na kusini mwa Afrika cha kudhibiti Panya na matumizi yake katika kunusa (ACE IRPM & BTD).***

Mkurugenzi Mkazi wa Benki ya Dunia Nchini Tanzania Bw. Nathan Belete amepongeza Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kutumia fedha zilizotolewa na Benki hiyo na kuahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuendeleza matokeo mazuri yaliyopatikana.

Hayo aliyasema wakati akizungumza na Uongozi na Watafiti wa Chuo hicho mara baada ya kupokea mawasilisho ya utekelezaji wa fedha zilizotolewa na Benki hiyo katika utekeelezaji wa miradi kwenye Taasisi ya afya moja inayoshughukikia magonjwa ambukizi kusini mwa jangwa la sahara (SACIDS), Mradi wa HEET na Kwenye kituo cha umahiri cha mashariki na kusini mwa Afrika cha kudhibiti panya na matumzi yake katika kunusa (ACE IRPM & BTD).

“Kwa kutambua mchango wa elimu kama mtaji wa binadamu ndio maana Benki ya Dunia tumeweka swala la elimu kama kipaumbele kwenye utekelezaji wa miradi yetu hivyo nitumie nafasi hii kuahidi Wizara ya Elimu pamoja na SUA kuwa tutaendelea kutoa ushirikiano katika kuteleza miradi kama hii ambayo inaleta tija kubwa kwenye maendeleo ya wananchi na Taifa” alisema Bwana Belete.

Bwana Belete alipongeza kazi nzuri inayofanywa na SUA katika kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali za taifa na kuahidi kushirikiana na Chuo hicho kwenye kusaidia ongezeko la udahili wa Wanafunzi kutokana na takwimu kuonesha udahili nchini Tanziania upo chini ikilinganishwa na nchi jirani.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi wa Elimu ya Juu, Dkt Keneth Hosea akitoa salamu za Wizara ya Elimu ameiomba Benki ya Dunia kuona uwezekano wa kuongeza fedha kwenye miradi hiyo ili kazi nzuri iliyofanywa na miradi kwenye vituo hivyo vya umahiri iendelezwe zaidi.

“Kwakuwa kupitia mradi wa HEET unakwenda kuongeza nguvu kwenye kampasi 15 mpya kwenye vyuo mbalimbali vya umma nchini tunaomba Benki ya Dunia itusaidie kuongeza fedha kwenye eneo la Mafunzo kwa wa-

***Inaendelea Uk. 5***

**Ardhi ni Hazina**



*Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda akitoa salamu za SUA.*

nataaluma pamoja na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwenye maabara zetu" aliomba Dkt. Hosea.

Awali Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda alisema mchango wa miradi hiyo miwili ya SACIDS na (ACE IRPM & BTD iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia ni mkubwa sio tu kwa Tanzania bali kwa bara la Afrikakwani tafiti zake zinagusa Afrika.

"Naomba nitumie nafasi hii kushukuru sana msaada tunaoupata kutoka Serikali yetu na Bank ya Dunia ambayo inasaidia chuo kwenye kutekeleza majukumu yake na kupitia Mradi wa HEET tunawekeza katika shamba letu la Miti huko Madaba ili ndani ya kipindi cha miaka mitano tuongeze mapato yetu ya ndani ya Chuo na kupunguza utegemezi" alisema Prof. Chibunda.

Katika mkutano huo Chuo kilipata nafasi ya kutoa mawasilishao mbalimbali ikiwemo Historia, Kazi na mafanikio ya Chuo toka kuanzishwa kwake iliyowasilishwa na Naibu Mkamu Mkuu wa Chuo Taaluma Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala ambaye alieleza namna Chuo kinavyotekeza majukumu yake.

Aidha, Mawasilisho mengine ni Utekelezaji wa Taasisi ya afya moja inayoshughukikia magonjwa ambukizi kusini mwa jangwa la Sahara (SACIDS) lililowasilishwa na Prof. Gerald Misinzo, Wasilisho la Mradi wa HEET lililowasilishwa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango Utawala na Fedha Prof. Amandus Muhairwa na Mratibu wa Mradi huo Dkt. Winfred Mbungu na Wasilisho la Kituo cha Umahiri cha Mashariki na Kusini mwa Afrika cha Kudhibiti Panya na matumzi yake kanitika kunusa (ACE IRPM & BTD kutoka kwa Prof. Appiah Masawe.

Baada ya mawasilisho hayo Mkurugenzi huyo Mkazi wa Benki ya Dunia Nchini Tanzania Bw. Nathan Belete pamoja na ujumbe wake walipata nafasi ya kutembelea kuona vituo hivyo na kazi zinazofanyika na kuona namna fedha walizotoa zilivyosaidia kufanyika kwa tafiti zenye faida kubwa kwa taifa na Afrika.



*Naibu Mkamu Mkuu wa Chuo Taaluma Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu Prof. Maulid Mwatawala akitoa salamu na Historia ya Chuo.*



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa akiwasilisha sehemuya utekelezaji wa Mradi wa HEET.*

**Ardhi ni Hazina**

# SUA yasaidia wenye mahitaji maalum



Jamii imetakiwa kuwa na utamaduni wa kutembelea na kuyagusa maeneo mbalimbali ya watu wenye mahitaji maalum ili kuwa na ustawi wa wananchi katika makundi mbalimbali.

Wito huo ulitolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo upande wa Mipango, Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa wakati akizungumza na waalimu na baadhi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Kauzeni iliyopo Manispaa ya Morogoro Leo tarehe 24 Agosti, 2023.

Prof. Muhairwa alieleza kuwa kwenye jamii kuna baadhi ya makundi yanahitaji misaada ya namna tofauti tofauti ili kuweza kujikwamua katika vikwazo wanavyokabiliana navyo, akisema kuzitembelea jamii hizo ni kutengeneza ustawi wa kila kundi.

"Tunafahamu sisi tuko hapa lakini kuna maeneo mengine wanahitaji misaada kama hii, tukiwa na utamaduni wa kila mmoja wetu kuyatembelea maeneo kama haya tutakuwa na ustawi mzuri na umoja miongoni mwetu", alisema Prof. Muhairwa.

Mkurugenzi Menejimenti ya Rasilimali Watu na Utawala Bw. Peter Mwakiluma akiongea katika tukio hilo alieleza kuwa wametoa msaada huo kama sehemu ya kuwa karibu na jamii pia ni takwa na serikali ambapo inazitaka Taasisi zote kuwa na wiki ya utumishi kwa kuigusa jamii na kutoa elimu kwa watumishi katika masuala mtambuka ya kiutumishi.

Mwakiluma aliongeza kuwa msaada ambao wametoa una thamani ya zaidi ya Tsh 5,200,000 ukijumuisha viti mwendo (Wheelchair), magodoro, mchele, maharage, sukari, vifaa vya kufundishia, mafuta ya kupikia n.k

Mkwinda Said Chuma Mwalimu wa wanafunzi wenye mahitaji maalum shuleni hapo aliishukuru SUA kwa kutoa msaada huo akisema utasaidia katika kupunguza changamoto zinazoikabili shule hiyo ikiwemo katika kurahisisha ufundishaji wa wanafunzi hao.

Aidha, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kauzeni, Yunus Idd Hamis, 12, pamoja na kukishukuru Chuo kwa niaba ya wanafunzi wengine pia aliwaomba wadau wengine kuendelea kuwasaidia kwani nao wanahitaji kusoma kwenye mazingira rafiki kama walivyo wengine.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo tangu mwaka 2019 kimeendelea kuadhimisha wiki ya utumishi kwa kushiriki shughuli mbalimbali za kijamii ikiwemo kutoa misaada na kufanya usafi.

**Ardhi ni Hazina**



**Prof. Raphael Chibunda**
**Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.**

# Prof. Chibunda aongea na Watumishi wa SUA Kampasi ya Edward Moringe

Muendelezo wa vikao vya Menejimenti, Ndaki pamoja na Idara mbalimbali katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo umeendelea kufanyika ambapo Makamu wa Mkuu wa chuo hicho Prof. Raphael Chibunda amekutana na wafanyakazi wa Idara zote za jengo Kuu la utawala, Farm, Shule Kuu ya Uchumi na Biashara ili kukumbushana baadhi ya Miongozo, Sheria na Taratibu katika utumishi wa Umma vile vile kusikiliza maoni kwa lengo la kuboresha Taasisi.

Muendelezo wa vikao hivyo vilifanyika Kampasi Kuu ya Edward Moringe Sokoine mjini Morogoro na kikao hicho ni cha nne tangu kuanza kwa vikao hivyo Agosti 14, 2023

Prof. Raphael Chibunda alisema mwaka umeisha na kumekuwa na mambo mengi yametokea na SUA ni Chuo cha umma ambapo kinaongozwa na Sheria na Taratibu mbalimbali vile vile kuna miongozo kadhaa inatolewa na Serikali Kuu na ile inayopitishwa na Baraza la Chuo hivyo wanadhani kitu chema wao kama viongozi baadhi ya hiyo miongozo au mabadiliko kuweza kupata nafasi ya kuieleza kwa wafanyakazi.

"Tupo hapa kama wafanyakazi kutathmini kile ambacho tumekifanya kwa mwaka ulioisha, wapi panahitaji marekebisho na kipi kinahitaji maboresho hivyo ni nafasi ya kila mmoja kuleta malalamiko, mawazo na hata maoni lengo likiwa ni kujenga" alisema Prof. Raphael Chibunda

"Lengo lingine kubwa ni kushukuru na kupongeza wafanyakazi hasa baada ya nafasi kubwa ya kutimiza majukumu ya Chuo chetu hasa katika muhula wa masomo ulioisha, kinachohitajika sasa ni nguvu na ubunifu mpya wa utendaji kazi ili kufikia malengo tuliyojiwekea", alieleza zaidi Prof. Chibunda.

Kwa upande wake Prof. Maulid Mwatawala Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalam alisema kuwa kwenye upande wa ufundishaji wameingia katika mfumo mpya wa ufanyaji mitihani ambapo katika mfumo huo mitihani yote itafanyika katika muhula husika hivyo hakutakuwepo na mitihani ya mwezi wa kumi hivyo mwanafunzi atatakiwa kufanya mtihani mara moja na kuruhusiwa kurudia mara mbili pale ambapo amefeli.

Alisema faida ya Mfumo huo ni kuwa Wanataaluma wanapata muda wa likizo au kupumzika ili kuendelea na majukumu yao mengine ya kitaaluma kama kufanya Tafiti. Vilevile kutengeneza ratiba yake ya muhula unaofuatia hata hivyo kwa upande wa mwanafunzi hata kama kuna baadhi ya masomo amefeli na ana GPA ya kutosha hakuna kitakacho mzuia kusonga mbele kwakuwa atayabeba masomo yake na kuendelea mbele.


"Hii ina maana kuwa tunatoka katika mfumo wa temu kwenda kwenye mfumo wa muhula (semister) ambapo mfumo wa temu ulikuwa unatumia mitihani ya marudio (suplimentary exams) kwamba ukiwa na sup ukaifanya ukafeli unaondolewa chuoni (disqualified) na ukiwa umefaulu unaendelea mbele yaani huwezi kwenda mbele bila kufaulu masomo yote hata liwe somo moja", alisema Prof. Maulid Mwatawala.

Naye Prof. Amandus Muhairwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Mipango, Fedha na Utawala amesema Wana mipango mipya ya maendeleo kwa mwaka 2023/2024 ikiwemo ujenzi pamoja na ukarabati wa majengo.



## Picha mbalimbali za Watumishi wa SUA wakati wa kikao cha Makamu Mkuu wa Chuo na Watumishi hao


Prof. Amandus Muhairwa
Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Mipango, Fedha na Utawala).


Prof. Maulid Mwatawala
Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu.









**Ardhi ni Hazina**

# Msitu wa Hifadhi Mazumbai SUA kuendelea kupokea Watafiti, Wanasayansi na Watalii



***Mhifadhi wa Msitu wa Mazumbai, Tanga akitoa maelezo kwa watalii na watafiti wakiwa kwenye msitu huo.***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeendelea kupokea Watafiti, Wanasayansi na Watalii kutoka nchi mbalimbali duniani wanaokwenda kujifunza, kufanya tafiti na utalii juu ya masuala mbalimbali ya Misitu na Viumbe wengine wengi kwenye Msitu wa Hifadhi Mazumbai unapatikana Jimbo la Bumbuli Mkoani Tanga. Msitu huo haujawihi kuguswa toka miaka ya 1800 enzi za ukoloni wa Mjerumani.

Hayo yalibainishwa na Mhadhiri Msaidizi na Kaimu Msimamizi wa Msitu huo na kituo hicho cha Mafunzo cha SUA, Mhifadhi Bw. Chamalindi Bugingo Muriga wakati akiongea na Waandishi wa habari waliokwenda kutembelea kituo hicho kuona vivutio mbalimbali vya kipekee na viumbe vinavyopatikana kwenye msitu huo.

‘‘Kazi kubwa inayofanywa na Menejimenti ya SUA katika kutunza msitu huu wa asili ndio inayowavutia wanasayansi wengi duniani kuona hapa ndio mahali sahihi kwa wao kuja kujifunza na kufanya tafiti za misitu na viumbe hai mbalimbali wa kipekee wanaopatikana kwenye msitu wetu, Msitu huu haujawahi kuguswa kwa shughuli yoyote ya kibinadamu zaidi ya miaka 200 na hivyo kupelekea kuwa na miti mikubwa ambayo pengine haipo maeneo mengine duniani’’, alieleza Mhifadhi Chamalindi.

Aidha alisema, kutunzwa vizuri kwa msitu huo kunasaidia kuwa sehemu nzuri ya benki ya mbegu za miti mingi ya asili ikiwemo mimea dawa, Miti ya mbao na matunda ambayo huwezi kupata kwenye misitu mingine ya asili nchini na hii kuwa kimbilio la watafiti wengi wa masuala ya misitu, ndege, uyoga, wanyama, vyura na vinyonga.

‘‘Kwenye Msitu huu kuna miti yenye maumbo mbalimbali ya kuvutia ikiwemo miti aina ya Mibokoboko Entandrophragma deiningerii yenye mizizi mikubwa zaidi ya mita 2 kutoka ardhini ambayo imetengeneza ukuta kama nyumba, mingine mikubwa ambayo kiuno chake kuweza kuukumbatia hadi muungane watu wazima saba, na mingine yenye Mtonho/Mtonto Cylicomorpha parviflora ‘‘ alifafanua Mhifadhi Chamalindi.

Kwa upande wake Rasi wa Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Dkt. Agnes Sirima alisema msitu huu wenye ukubwa wa hektari 320 ni fahari ya Tanzania kwa kuwa ndio msitu pekee mkubwa na ulioshona ambao unamilikiwa na SUA.

‘‘Pamoja na kutumiwa na Wanasayansi na Watafiti wengi duniani lakini tunautumia kwenye kufundisha Wanafunzi wa Shahada mbalimbali za Misitu, Uhifadhi, Mazingira na Utalii na hivyo kituo hiki kuwa na mchango mkubwa kwa Chuo kwenye kutoa Mafunzo kwa Vitendo kwa wanafunzi wetu’’, alieleza Dkt. Sirima.



***Msitu wa Hifadhi wa Mazumbai, Tanga.***

# SUA yafanya ziara ya Mafunzo nchini India



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Upande wa Mipango Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa akiwasilisha wasilisho kuhusu shughuli zinazofanywa na SUA.*

Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Upande wa Mipango Fedha na Utawala Prof. Amandus Muhairwa ameongoza timu ya baadhi ya wataalamu kutoka (SUA) kufanya ziara ya kimafunzo na kuendeleza ushirikiano na Chuo Kikuu cha Lala lajpat Rai (LUVAS) cha nchini India.

Katika ziara hiyo walipata nafasi ya kutembelea maeneo mbalimbali ikiwemo eneo la IIT ROORKEE ambalo linashughulika na masuala ya Rasilimali za Maji na Mitaala ya Kimataifa na kutumia nafasi hiyo kufanya pia mawasilisho kuonesha kazi mbalimbali na mafanikio ya Chuo.

Ziara hiyo ilifanikishwa na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET).









# SUA yaanzisha mashirikiano na Chuo Kikuu CCS Haryana nchini India



***Profesa Bernard Chove na Profesa Baldev Kamboj wakisaini Hati ya Mashirikiano kati ya SUA na CCSHAU jijini Dar es Salaam.***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kimeanzisha mashirikiano na Chuo Kikuu cha Chaudhary Charan Singh Haryana cha Kilimo Hisar (CCSHAU) ili kuimarisha shughuli za utafiti, kubadilishana wanataaluma na wanafunzi na kuanzisha mafunzo ya pamoja kati ya taasisi hizi. Hafla ya uzinduzi wa mashirikiano hayo ilifanyika katika viwanja vya Maonesho vya Sabasaba jijini Dar es Salaam siku ya Jumanne tarehe 11 Julai 2023.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, aliyekuwa Rasi wa Ndaki ya Kilimo kutoka SUA, Profesa Bernard Chove ambaye alimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo wa SUA alisema Tumejipanga vema kuona Vyuo vyetu vya SUA na CCSHAU vinaendeleza mahusiano ya kuinua taaluma, tafiti na ugani ili kuhakikisha Elimu ya Juu inakuwa chachu ya maendeleo nchini Tanzania na India.

Kwa upande wa Chuo Kikuu cha CCS Haryana cha Kilimo, Makamu wa Mkuu wa chuo hicho, Profesa Baldev R. Kamboj alisema leo ni siku ya furaha kwangu na wanajumuiya wa CCSHAU kushuhudia kuanzishwa kwa mashirikiano kati ya Vyuo vyetu, makubaliano yetu yasiishie kusaini makaratasi bali tuyaweke katika utekelezaji mapema kadri iwezekanavyo.

Katika kuhakikisha utekelezaji wa mashirikiano unaanza mara moja, Chuo Kikuu cha SUA kitapokea wanataaluma wa fani ya Uhandisi wa Kilimo ili kuja kushirikiana na wenzao wa SUA katika kutoa mafunzo kwa wanafunzi wa SUA. Pia vyuo vikuu hivi vimekubaliana kufanya juhudi katika kuanzisha Kituo cha Pamoja cha Atamizi na Teknolojia nchini Tanzania ili kuhakikisha wanafunzi wa Tanzania na India wanapata mafunzo kwa vitendo na hivyo kuwaandaa kikamilifu katika upatikanaji wa ajira baada ya mafunzo yao.

Aidha Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo hivi karibuni kinatarajia kutuma timu ya Menejimenti nchini India kutembelea na kujifunza zaidi kutoka kwa wenzao wa CCSHAU na kubainisha maeneo zaidi ya mashirikiano katika kutekeleza makubaliano yao.

# SUA yawajengea uwezo Wahadhiri juu ya uandaaji Mitaala Mtandao

*"Tunatoa mafunzo haya ili tuweze kuwa na mitaala itakayoongeza ubora wa wahitimu wetu na kuendana na maendeleo ya sayansi na teknolojia"*

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kupitia Mradi wa HEET kimeanza kutoa mafunzo kwa Wakuza Mitaala wa Chuo hicho ili kuwajengea uwezo wa uandaaji wa mitaala ya kisasa itakayoendana na wakati uliopo.

Akizungumzia mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uratibu wa Uboreshaji na Ukuzaji wa Mitaala SUA Dkt. Jamal Jumanne amesema chini ya Mradi wa HEET unaotekelezwa hapa Chuoni watakuwa na Mitaala ambayo itakuwa na uwezo wa kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi ikiwemo kutumia njia ya mtandao na njia ya mchanganyiko (blended).

Dkt. Jamal ameeleza kuwa kupitia mitaala ambayo inaundwa, Chuo kitakuwa na uwezo wa kudahili idadi kubwa ya wanafunzi ambao watakuwa na uwezo wa kujifunza katika njia rahisi ambayo itamruhusu kusoma akiwemo sehemu yoyote mbali na kukaa darasani.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt. Salome Maro amesema madhumuni ya mafunzo hayo ni kuhakikisha kunakuwa na vipengele sahihi hasa katika kutoa mafunzo kwa njia ya mtandao hivyo ni matumaini kuwa mafunzo hayo yatawaandaa vyema wakuza mitaala kuwa na ujuzi katika kuandaa programu zenye tija ili kukisaidia Chuo kuwa na uwezo wa kuandaa Wahitimu wenye sifa na mahitaji ya sasa.



*Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo wakiwa katika mkutano mmoja wapo wa kuandaa mitaala mtandao uliofanyika Jengo Mtambuka la Mafunzo, Kampasi ya Edward Moringe.*



# SUA YAZINDUA MAGARI MATATU KWA AJILI YA KURAHISISHA UTEKELEZAJI WA MRADI WA HEET




***Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET SUA, Dkt. Winfred Mbungu akiyatazama magari baada ya kuzinduliwa.***

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) imezindua magari matatu, mawili aina ya Double Cabin na moja aina ya Land Cruiser Hardtop kwa lengo la kusaidia kurahisisha shughuli za mradi huo kwa ufanisi mkubwa ikiwemo ufuatiliaji wa masuala ya ujenzi.

Alibainisha hayo Dkt. Winfred Mbungu, Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET SUA wakati akizungumza na SUA-MEDIA kwenye uzinduzi wa magari hayo Kampasi ya Edward Moringe Mjini Morogoro.

Alisema wamekuwa na shughuli nyingi ambapo zingine zitaenda kuanza hivi karibuni hasa za kufuatilia mambo mengi ya ujenzi ambapo wamekuwa wakihitaji usafiri na mara nyingi wamekuwa wakitumia magari ambayo yamekuwa pia na shughuli nyingine chuoni hapo hivyo magari hayo yaliyozinduliwa yataenda kurahisisha kazi kwa sababu ni mahususi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi.

Dkt. Mbungu alisema wanapenda kutoa shukurani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Fedha hizo walizozipata za Mradi wa HEET kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambazo zimewezesha kupelekea SUA kununua hayo magari ambapo wanatumaini yataenda kuboresha Mazingira ya watu kujifunzia pamoja na kufundishia na pia kuboresha kiwango cha wahitimu wao ambao watamaliza SUA.

"Hii ni seti mojawapo lakini tuna magari mengine tunayatarajia hapo baadae ambayo mengine yatatumika kwa mafunzo kwa vitendo zaidi kama vile mabasi pamoja na minbus kwa ajili ya kurahisisha shughuli za mafunzo kwa vitendo lakini haya tuliyoyazindua ni kwa ajili ya kufanikisha shughuli za kufuatilia utekelezaji wa Mradi alisema", Dkt. Mbungu.

**Ardhi ni Hazina**



*Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Raphael Chibunda akikata utepe kuashiria uzinduzi wa magari ya Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi katika Jengo la Utawala Kampasi ya Edward Moringe.*




## Picha za matuki mbalimbali katika uzinduzi wa magari ya Mradi wa HEET





# Jimbo Katoliki Tanga, kuanzisha ushirikiano na SUA katika Kilimo

***Mkuu wa Idara ya Sayansi ya Wanyama, Ukuzaji Viumbe Maji na Nyanda za Malisho Prof. Anthony Sangeda akiwaeleza jambo wageni kutoka Jimbo Katoliki la Tanga kuhusu Kitengo cha Uchumi wa Buluu.***

Jimbo Katoliki la Tanga kupitia mradi wao wa kuanzisha Shule ya Sekondari limeanzisha ushirikiano wa awali na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo katika nyanja ya kilimo ili iweze kuandaa wanafunzi bora.

Mkuu wa Idara ya Sayansi ya Wanyama, Ukuzaji Viumbe Maji pamoja na Nyanja za Malisho Prof. Anthony Sangeda kutoka SUA akiongea na SUAMEDIA wakati wa mapokezi ya ugeni huo tarehe 12 Septemba 2023, ameeleza kuwa ujumbe walioupokea unalengo la kujifunza namna SUA inavyofundisha programu za Kilimo kwa ubora ili nao wakaboreshe kwenye shule wanayokusudia kuianzisha.

Prof. Sangeda amesema ushirikiano huo baina ya SUA na Jimbo Katoliki la Tanga unakusudia kuifikisha dhana ya kilimo kwa vijana wadogo kwani watajua mambo ya msingi ya kujifunza kwa muda husika na wanafunzi watakuwa na uwezo wa kujiendeleza katika kilimo kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

“Kimsingi kabisa wageni hawa wana mradi ambao wanauanzisha katika jimbo katoliki la Tanga ambayo ni sekondari ya vijana na wanapenda iwe ya mfano kwa nchi hii kwa ajili ya kujifunza kwa vitendo mchakato wa kilimo kwa hiyo wameona ni vyema wajifunze namna sisi (SUA) tunafanya”, alisema Prof. Sangeda.

Kwa upande wake Padri Gerald Theodol Kabarega kutokea Jimbo Katoliki la Tanga amesema kuwa katika mradi wao wa shule, wameona ni vyema kuwa na sehemu moja wapo ya kilimo ambayo itakuwa chini ya uangalizi wa Chuo Kikuu cha Kilimo ili waweze kujifunza mambo yahusuyo kilimo ambapo yatawasaidia kupata shauku ya kujiendeleza katika masomo ya kilimo hapo baadaye.

Padri Kabarega ameongeza kuwa kabla ya kuwa na shule ya sekondari waliafikiana wasiwe na shule ya sekondari yenye masomo ya nadharia pekee wakaona muhimu kupata uzoefu wa namna ya kufundisha wanafunzi masomo ya kilimo kwa vitendo kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla.

Mbali na Padri Gerald Kabarega ambaye ni msimamizi wa mradi wa kuanzisha shule hiyo ya sekondari kwa Jimbo hilo pia alikuwa ameambatana na Mratibu wa Mradi Bw. John Kibilango wa Tanzania na Bw. Klaus kutoka nchini Ujerumani.

**Ardhi ni Hazina**

# Baadhi ya picha za ziara ya wageni kutoka Jimbo Katoliki Tanga, walipotembelea maeneo mbalimbali ya SUA











# Serikali yaipongeza SUA kwa uzalishaji wa Wataalamuu wa mitambo ya kilimo

*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) akiongea wakati wa ziara yake katika Shule Kuu ya Uhandisi na Teknolojia ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.*

Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) kwa niaba ya Serikali amekipongeza Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kuiendeleza mitambo ya kilimo iliyotolewa na Serikali pamoja na uzalisha wa Wataalamu wa Mitambo hiyo.

Aliyazungumza hayo Septemba 15, 2023 akiwa Shule Kuu ya Uhandisi na Teknolojia iliyopo Kampasi kuu ya Edward Moringe alipofanya ziara chuoni hapo kufuatilia uhai wa vifaa vya kilimo (trekta) za URSUS zilizotolewa na Serikali kwa ajili ya kufundishia na kufanyia shughuli za kilimo kwenye mashamba ya mafunzo sambamba na kusaidia jamii kwa ujumla.

Dkt. Kijaji alisema kuwa Serikali kupitia wizara yake imeamua kufuatilia uhai wa trekta ambazo ziligawiwa miaka mitano iliyopita ambapo wameanza na SUA kwani kimekuwa kinara katika kuzalisha wahitimu bora katika sekta ya kilimo pamoja na kujiridhisha na uwepo wa wataalamu wa kuendesha mitambo hiyo.

"Sisi kama Serikali na hasa tuliopewa dhamana ya kuyasimamia Matrekta haya, tumesema tufike huku SUA hasa katika shamba tuone yale Matrekta mazima ni mangapi na yale ambayo yanachangamoto ni mangapi na nini kifanyike ili kuhakikisha wakulima wetu wananufaika na Mradi huu ambao ulileletwa kwa dhamira njema kabisa ya kuinua kilimo chetu ndani ya Taifa letu", alisema Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Kondoa vijijini.

Aidha, Waziri huyo alitoa wito kwa wakulima nchini hasa wale ambao walinunua trekta hizo kuangalia mafundi wanaowatumia ili ziweze kudumu kwa muda mrefu huku akiwaasa vijana wanaonufaika na Mradi wa BBT kukitembelea Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ili

*Inaendelea Uk. 18*

waweze kupata uzoefu zaidi katika shughuli za kilimo cha kisasa.

Kwa upande wake, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo Prof. Raphael Chibunda alimweleza Mheshimiwa Waziri kuwa SUA baada ya kubaini matumizi ya mitambo ya kilimo nchini yanaongezeka kwa kasi walishachukua hatua ya kuanzisha shule mahsusi ya kufundishia waendesha mitambo hiyo lengo likiwa ni kuhakikisha kilimo kinalimwa kwa tija hapa nchini.

Aliongeza kwa kuishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipatia SUA trekta ambazo zinaendelea kukisaidia Chuo katika kuboresha ufundishaji na utaoji wa huduma za kilimo kwa Wanajumuiya wa SUA na jamii kwa ujumla.

"Sisi kwa kuzingatia uzoefu mkubwa tulioupata sasa kwa kuwa na haya Matrekta, nipende kuwapa imani wale ambao wanamiliki haya Matrekta iwe kwa mkopo au kununua kama watakutana na changamoto kwenye matrekta hayo jambo la muhimu ni kutafuta mafundi ambao wanaufahamu wa injini za trekta ili waweze kurekebisha kwa ufanisi ili yafanye kazi kwa muda mrefu zaidi", alisema Prof. Chibunda.

*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) akipata maelezo toka kwa Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda.*








*Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb) akiwa juu ya trekta wakati wa ziara yake katika Shule Kuu ya Uhandisi na Teknolojia.*

# Picha za Watumishi wa Ndaki ya Uchumi na Stadi za Biashara wakiwa katika majukumu yao ya kila siku













# Ardhi ni Hazina







*Ndaki ya Uchumi na Stadi za Biashara*





**Ardhi ni Hazina**

# SUA, Japan yasaini makubaliano kukabiliana na magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu



*Dkt. Coletha Mathew (kulia) na Mshauri Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Dkt. Yumi Kirino (kushoto) wakisaini mkataba wa makubaliano ya kukabiliana na magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.*

Watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na watafiti kutoka Japan wamesaini Mkataba wa Makubaliano ili kujadili namna ya kutekeleza mradi unaohusiana na kukabiliana na magonjwa makuu mawili ambayo yanatoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu yanayojulikana kama ugonjwa wa kutupa mimba (Brucellosis) na Kifua Kikuu (Zoonotic Tubeculosis) kwa kutumia dhana ya afya moja.

Akizungumzia mkataba huo unaotekelezwa mkoani Morogoro na watafiti kutoka SUA kwa ushirikiano na Taasisi nyingine za Elimu ya Juu kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) na AMED, Dkt. Coletha Mathew, Mtafiti na Mhadhiri Mwandamizi wa Ndaki ya Tiba ya Mifugo na Afya ya Jamii katika Idara ya Anatomia na Patholojia amesema mradi huo ni muhimu kwa Chuo na Taifa kwani utaenda kukabiliana na magonjwa ambayo yapo katika jamii kwa muda mrefu.

"Sisi SUA tutafaidi kwa maana ya kwamba utafiti huo utazalisha machapisho ambayo yatakitangaza Chuo chetu lakini pia ni kupeleka huduma za ugani kwa jamii kwa hiyo wananchi watapata uelewa wa namna gani ya kukabiliana na magonjwa hayo", alisema Dkt. Coletha.


Kwa upande wake, Mshauri Mkuu wa Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Dkt. Yumi Kirino ameeleza kuwa ndani ya miaka mitano (kuanzia Julai 2024) ya utekelezaji wa mradi umechagua kwenda kuyafanyia kazi magonjwa hayo mawili ambayo yanaambukizwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu kwa sababu bajeti ya kuzuia aina hiyo ya magonjwa haijitoshelezi katika nchi nyingi.

Nae Katibu Tawala Msaidizi sehemu ya Uchumi na Sekta za Uzalishaji Ofisi ya Mkoa wa Morogoro, Dkt. Rozalia Rwegasira, ameeleza kuwa Mkoa ni wanufaika wa mradi huo kwani utakwenda kuwasaidia wananchi wa Mkoa wa Morogoro, kutambua magonjwa hayo na namna ya kujikinga.





**Ardhi ni Hazina**




***Mtafiti na Mratibu wa Wakifu wa Afya Moja wa SACIDS Prof. Gerald Misinzo akiwaeleza Waandishi wa Habari wa TBC (hawapo pichani) namana SUA wanavyoshirikiana na Serkali kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.***

# SUA Kushirikiana na Serikali Kukabiliana na magonjwa ya mlipuko

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimejipanga kuendelea kushirikina na Serikali katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko kwa kushiriki kufanya tafiti pamoja na kutumia mitambo ya kisasa ya kutambua vinasaba vya magonjwa.

Mtafiti na Mratibu wa Wakifu wa Afya Moja wa SACIDS Prof. Gerald Misinzo alieleza hayo wakati anaelezea namna SUA inavyoshirikiana na Serikali katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ambapo amesema kuwa kupitia ufadhili walioupata wa mitambo ya kisasa kutoka serikalini imeweza kusaidia kufundishia wanafunzi sambamba na kubaini magonjwa mbalimbali angalau kwa kipindi kisichozidi masaa 72 kama ilivyofanyika mkoani Kagera mapema mwaka huu.

Prof. Misinzo alibainisha kuwa baadhi ya vifaa ambavyo vimeongeza uwezo wa Chuo kukabiliana na magonjwa ni kifaa kinachojulikana kama kifaa cha uchambuzi wa vinasaba ambao unaweza kubaini vijidudu vinavyosababisha ugonjwa (Next Generation Sequence).

"Tukiweza kuufahamu ugonjwa katika maeneo ya utafiti tunarudi katika maabara na hiyo inasaidia kuudhibiti ugonjwa mapema, lengo ni kudhibiti kwenye kipindi kifupi ili kupunguza ugonjwa kusambaa", alisema Prof. Misinzo.




***Kifaa kinachojulikana kama kifaa cha uchambuzi wa vinasaba ambao unaweza kubaini vijidudu vinavyosababisha ugonjwa (Next Generation Sequence).***

# Picha mbalimbali za matukio ya michezo katika viwanja vya michezo vya Kampasi ya Edward Moringe












Kampasi ya Msitu wa
Mafunzo wa Olmotonyi, Arusha



Kampasi ya Msitu
wa Mafunzo Mazumbai, Tanga